**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Nne – Tarehe 13 Septemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

73. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

    Mwaka uliopita baadhi ya maeneo yalikumbwa na tetemeko dogo la ardhi yakiwemo maeneo ya Wete na Chake Chake.

    (a) Je, ni tahadhari zipi zinazochukuliwa katika kuhakikisha kuwa wananchi wetu wako salama hasa ukizingatia kuwa Zanzibar ni nchi ya visiwa.

    (b) Ni mazingatio yepi ambayo Serikali imekuwa nayo juu ya matukio ya matetemeko madogo ambayo yamewahi kutokea mara mbili kwa mwaka katika kipindi cha karibuni.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

45. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Serikali ya awamu ya saba ilianzisha kitengo cha uchunguzi wa hesabu za ndani (Internal Audit Unit).

    (a) Je, kitengo hicho kimeishia wapi.

    (b) Kama kipo, kwa nini hakiboreshwi zaidi.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

83. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Kwa kuwa Wilaya ya Chake Chake imepiga hatua katika maendeleo na idadi ya wakaazi, na kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi kuimarisha miundombinu mbali mbali katika Wilaya hiyo.

Je, ni lini Serikali italipandisha hadhi Baraza la Mji Chake Chake na kuwa Manispaa.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

29. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa miaka mingi Zanzibar tumekuwa hatufanyi vizuri katika tasnia ya michezo pamoja na kuwepo kwa mazingira mazuri kwa ajili ya michezo hususan mpira wa miguu au soka. Kwa kuwa mpira wa miguu wa ufukweni (Beach soccer) tayari umepanda chati katika medani ya kimataifa na tayari mashindano ya kimataifa ya kikanda yameanzishwa katika nchi mbali mbali ikiwemo Tanzania Bara. Na kwa kuwa mazingira ya Zanzibar ni mazuri kwa ajili ya mpira wa ufukweni.

(a) Je, ni timu ngapi zimeanzishwa kwa ajili ya mchezo huo hapa kwetu Zanzibar.

(b) Kama timu hizo zipo, Je, kuna ligi yoyote ya mashindano hayo.

(c) Kama hazipo, Je, ni lini zitaanzishwa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

124. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na jitihada za Serikali katika kufikisha huduma ya maji kwa wananchi, hadi sasa shehia zote za jimbo la Pandani zimeendelea kukumbwa na tatizo sugu la maji likisababishwa na ama uhaba au ubovu wa visima au uhaba wa matangi ya kuhifadhia maji ama kupatikana maji kwa siku chache au kwa masaa, kukosekana kwa bomba na mipira ya kusambazia maji, kutokuwepo kwa mashine ya kusukumia maji au machine kuwa ndogo.

(a) Je, ni lini visima viwili vilivyopo Msaani vitapatiwa mashine ili ziweze kusambaza maji katika maeneo yanayovizunguka.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza na kufukia matangi ya kuhifadhia maji katika shehia za jimbo la Pandani.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

44. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wananchi walio wengi wa Zanzibar wanazitegemea sekta za kilimo na uvuvi kujipatia kipato chao cha kila siku na kwa kuwa ndani ya Jimbo la Wingwi yako mabonde makubwa ya mpunga ya Koowe, Kwapongwe, Chwaka Kijichame na Ukele.

Je, Serikali itayaingiza mabonde hayo kwenye mfumo wa umwagiliaji ili kuwarahisishia wakulima wetu kufanya shughuli ya kilimo kileo zaidi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

111. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika kuharakisha maendeleo sawa na ya haraka katika nchi, mwishoni mwa miaka ya tisiini Serikali iliruhusu mitandao ya simu za mkononi Zanzibar. Hata hivyo, tokea miaka hiyo kumekuwa na usumbufu wa mawasiliano katika sehemu nyingi za jimbo la Pandani kutokana na ukosefu wa minara ya mawasiliano ya simu kukidhi mahitaji ya jimbo, hasa kwa vile mahitaji yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku na idadi ya watumiaji ikiongezeka.

(a) Je, ni kwa kipindi gani Serikali huyataka makampuni yanayotoa huduma za simu za mkononi kutathmini mahitaji mapya ya minara ya simu ili kukidhi mahitaji ya sehemu husika.

(b) Ni lini minara mipya ya nyongeza itasimamishwa katika maeneo ya jimbo la Pandani ili kukidhi mahitaji mapya ya simu za mkononi na kuondoa usumbufu kwa watumiaji.

119. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali imekuwa ikijitahidi vya kutosha kuboresha huduma za viwanja vya ndege. Hata hivyo, katika viwanja vya ndege vya Zanzibar, Unguja na Pemba, kumekuwa na usumbufu kwenye huduma za usafiri wa teksi hasa kwa watu wasio wageni.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuboresha na kurasimisha huduma za teksi na kuratibu bei sahihi za safari kutoka viwanja ndege kwenda sehemu tofauti.

(b) Je, kuna bei elekezi zinazotambulika za huduma za teksi kutoka viwanja vya ndege kwenda sehemu tofauti za miji na vijiji vya Unguja na Pemba.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

11. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hivi karibuni Serikali ilifanya maamuzi juu ya kuzirejesha sekta zilizogatuliwa kwenda kwenye Wizara husika. Jambo hili linatokana na uwezo mdogo wa Serikali za Mitaa kuziendesha sekta hizo ikiwa ni pamoja na ukosefu wa fedha.

Tokea utekelezaji huo kuanza kwa hatua za sasa Je, kumetokea mabadiliko gani ya ufanisi kwa sekta ya elimu tukilinganisha na awali.

64. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Matokeo ya mitihani ya taifa Zanzibar bado hayaridhishi na skuli nyingi hazifanyi vizuri katika kidato cha nne na sita.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuimarisha miundombinu mizuri kama vile Dahalia ili wanafunzi wasome katika mazingira ya utulivu.

(b) Je. vitabu na vifaa vya maabara vinapatikana kwa wakati.

(c) Wizara wanawasaidiaje walimu katika kuwajengea uwezo na mbinu mpya za ufundishaji.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

125. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kituo cha Afya cha Pandani na Kituo cha Afya cha Kiungoni ndani ya jimbo la Pandani vimekuwa vikihudumia wagonjwa kutoka ndani na nje ya jimbo la Pandani na kumekuwa na ongezeko kubwa la watu wanaotegemea huduma za vituo hivyo.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuvipandisha hadhi vituo hivyo vya afya na kuviongezea uwezo wa kutoa huduma zikiwemo magari ya kubebea wagonjwa wa dharura.

(b) Je, ni vigezo vipi na utaratibu gani wa kukipandisha hadhi kituo cha afya hadi kuwa hospitali ya kujifungulia.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

107. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika miaka ya hivi karibuni, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imekuwa ikifanya maonyesho mbali mbali ya biashara yakiwemo yaliyofanyika katika viwanja vya Kisonge Michenzani. Hata hivyo, eneo hilo kabla ya maonyesho hayo kulikuwa kunafanyika soko la Jumapili "Sunday Market" ambayo wajasiriamali wengi hasa kinamama walikuwa wakiuza bidhaa zao.

(a) Kufuatia kuondoshwa kwa soko hilo la Jumapili, Je, wajasiriamali hao wamepelekwa wapi kwa sasa.

(b) Je, watu wanaoshiriki maonyesho hayo wanatakiwa kulipa kiasi gani cha fedha za ushiriki.

(c) Je, fedha hizo baada ya makusanyo zinapelekwa wapi.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

89. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia awamu zake zote tokea Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964, imeendelea kuchukua juhudi kubwa katika kuiendeleza miji mikubwa hapa nchini, ikiwa ni pamoja na mji wa Chake Chake, ambao mkubwa na ndio unaotoa sura halisi ya kisiwa cha Pemba. Hata hivyo, mji huu wa Chake Chake hauendelezwi kama vile Serikali ilivyochukua juhudi za kuiendeleza miji mbali mbali hapa Unguja, kama vile Fumba, Kwahani, Mbweni na miji mengine ya kisasa.

(a) Je, ni lini Serikali itaujenga mji wa Chake Chake kuwa mji wa kisasa kama ilivyojenga kwenye maeneo mbali mbali hapa Unguja.

(b) Kwa kiasi gani Serikali inaendelea kuudumaza mji wa Chake Chake kwa kutouendeleza kwa majengo ya kisasa, kama ilivyofanya Fumba, Mbweni na Kwahani Unguja.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

100. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kununua meli mbili za uvuvi kwa lengo la kuendeleza uchumi katika sekta ya uvuvi nchini.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichozalishwa tokea meli hizo kuanza shughuli za uvuvi.

(b) Je, kupitia meli hizo tumeweza kutengeneza ajira ngapi kwa vijana wa Zanzibar.

(c) Je, soko gani linalotumiwa kuuza samaki baada ya meli hizo kukamilisha shughuli zake za uvuvi.

## III. HOJA ZA SERIKALI

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na Mambo mengine yanayohusiana na hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**13 Septemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**